Hukumu Au Usihukumu

na

Ellis P. Forsman

Hukumu Au Usihukumu

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Hukumu Au Usihukumu

Math. 7:1-6

Kipindi fulani cha nyuma ndugu alikuja kwangu na neno. Mshiriki mwingine alimpa orodha ya maandiko yanayohusu somo la "Usihukumu" na alimtaka atoe hotuba kwa kutumia maandiko haya. Mtu huyu alitaka tu "kuadhibu" wengine kwa sababu walikuwa wanamhukumu. Mtu aliyekuja kwangu akaniambia hakujisikia vizuri kwa kutoa hotuba hii, kwa hiyo nikasema nitaongelea somo hili, lakini nikajifikiria mwenyewe sitatumia tu mistari iliyochaguliwa pekee katika somo hili.

Tatizo moja lililokuwa katika orodha hii ya maandiko ni kwamba ilikuwa inaegemea upande mmoja, hivyo ikaleta mtazamo tofauti na kile Bwana alichosema kuhusu somo hili.

Tatizo lingine ni kwamba iliandaliwa kwa sababu ambazo si nzuri. Mtu huyu alitaka kutumia maandiko ili "kuadhibu" wengine. Msemo uliopendwa na watu wengi ni "*Usihukumu, nanyi msije mkahukumiwa".* Hii mara nyingi inanukuliwa kama jibu wakati ambapo mtu anaonyesha dhambi au makosa ya mtu fulani. Swala ni kwamba tusije tukahukumu kwa kile tunachokiona kwa wengine.

Je hiyo ni kweli? Hicho ndicho Yesu alimanisha aliposema hivyo? Je hatutafanya hukumu ya maadili kuhusu mema na mabaya yaw engine? Tukiona makosa kwa wengine, je hatuwezi kuitaja?

Nina shawishiwa kwamba kauli ya Yesu maranyingi inatumika vibaya, hiyo Yesu alifundisha.....

- Kuna nyakati ambazo tunapaswa kuhukumu.
- Kuna wakati mwingine ambao ni muafaka wa kutaja makosa kwa wengine.

"Kuhukumu au Kutokuhukumu", hilo ndilo swali lililoko mbele yetu. Jibu sahihi linatoka katika mtazamo wa karibu wa maneno ya Yesu katika Math. 7:1-6. Kwanza kabisa angalia jinsi maneno yake yanavyotumika mara nyingi vibaya:

Kataza aina yo yote ya hukumu?

Maneno yake maranyingi yanatumika kukataza aina "zote" za hukumu; kama vile dharau au ubaguzi wo wote – kama kuonyesha kosa kwa mtu fulani, hatakama ni kweli "inajenga" ubaguzi, kama vile zoezi la

nidhamu ya kanisa. Kufanyia zoezi nidhamu ndiyo inahitaji "hukumu" wengine katikamaadili yao au hali yao ya kiroho.

Kwa vile "hukumu" kama hiyo inajumlisha, baadhi wanahisi mistari kama 1-2 inaondoa hali yo yote ya nidhamu ya kanisa, kama yale yanayochimbua wale wanaofundisha uongo.

Inahitajika kufanya hukumu ili kujua kama mtu anafundisha uongo. Kwa hiyo, watu wengine, kwa kuzingatia mistari ya 1-2, wanaamini kwamba hatuwezi kuongea dhidi ya wale wanaofundisha uongo.

Je hicho ndicho Yesu alimaanisha? Lazima tunyamaze tunapoona watu wanakuwa katika makosa, wakileta matusi juu ya jina la Kristo, au kwa ubaya zaidi wakifundisha uongo? Hebu nipendekeze kwamba Yesu hakutupilia mabali aina "zote" za hukumu.

Angalia mazingira ya "karibu" ambayo yanafafanua kwamba hukumu "sahihi" inapaswa ifanyike. Math. 7:6, *"Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, wakageuka na kuwararua."*

Hii inaonyesha kwamba hukumu inatakiwa ifanyike kwamba ni wakina nani walio "*mbwa*" na "*nguruwe*" ni wakina nani. Vinginevyo, tutajuaje ni wakati gani hatupaswi kuwapa "*mbwa*"? Au, tutajuaje ni wakati gani hatupaswi kutupa lulu zetu mbele za *"nguruwe"*?

Math. 7:15-20, *"Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. Mtawatambua kwa matunda yao. Je! Watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika kibaruti? Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri, na mti mwovu huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri. Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni. Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua.*

Hii inamaanisha kwamba tunatakiwa tutowe hukumu kwa kuangalia ni nani aliye mwalimu wa uongo ("*Kwa matunda yao mtawatambua*").

Zingatia mazingira ya "ufunguo" inayozungumzia nyakati ambazo hukumu inatakiwa <u>lazima</u> ifanyike! Yesu alisema katika Yohana 7:24, "*Basi msihukumu hukumu ya macho tu, bali ifanyeni hukumu iliyo ya haki."*

Wakristo wana majukumu ya "Kuhukumu wale walioko ndani" kanisa la mahali pamoja. Paulo aliliambia kanisa la Korintho kwamba walikuwa na tatizo ambayo afadhali wangelishughulikia. Hakumwambia ndugu ye yote wa Kolosai, Filipi, Efeso, kanisa lolote la Galatia, au mahali popote pale waende Korintho kushughulikia swala hili. Aliliambia kanisa la Korintho kushughulikia swala hili.

1 Wakor. 5:9-13, *"Naliwaandikia katika waraka wangu, kwamba msichangamane na wazinzi. Sisemi msichangamane kabisa na wazinzi wa dunia hii, au na wenye kutamani, au na wanyang'anyi, au na wenye kuabudu sanamu, maana hapo ingewalazimu kutoka katika dunia. Lakini mambo yalivyo naliwaandikia kwamba msichangamane na mtu aitwae ndugu, akiwa ni mzinzi au mwenye kutamani au mwenye kuabudu sanamu au mtukanaji au mlevi au mnyang'anyi; mtu wa namna hii msikubali hata kula naye. Maana yanihusu nini kuwahukumu wale walio nje? Ninyi hamwahukumu hao walio ndani? Lakini hao walio nje Mungu atawahukumu. Ninyi mwondoeni Yule mbaya miongoni mwenu."*

Kila kusanyiko lazima lihukumu mambo ambayo yanatokea mbele yao linalohusu kusanyiko.

Tunafundishwa na Yohana (mtume wa upendo) "*kuzijaribu roho*" (inayohitaji kufanya hukumu, au sivyo?). 1 Yoh. 4:1, *"Wapenzi msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani."*

Hakuna mkanganyiko hapa, kwa sababu tunapoendelea na kifungu chetu, tunagundua kwamba Yesu anatafsiri ni "aina" gani ya hukumu anayolaani: kuhukumu wakati mtu ni kipofu kwa makosa yake mwenyewe.

Math. 7:3-5, *"Basi mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii? Au utamwambiaje nduguyo, niache nikitoe kibanzi katika jicho lako; na kumbe! Mna boriti ndani ya jicho lako mwenyewe? Mnafiki wewe, itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoa kile kibanzi katika jicho la ndugu yako."*

Yesu anasema kwamba ni makosa kwa ye yote kuhusika na kuweka angalizo lake katika kibanzi kilichopo katika jicho la ndugu, na kuliacha boriti ambalo lipo katika jicho lake mwenyewe.

Mara tu Paulo alipofundisha umuhimu wa mtu kujichunguza binafsi wakati anaposaidia wengine. Wagal. 6:1, *"Ndugu zangu mtu akighafilika katika kosa lolote, ninyi mlio wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo, <u>kwa roho ya upole</u>, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe."*

Yesu analaani kuhukumu pasipo huruma na upendo. Luka 6:36-37, *"<u>Basi iweni na huruma</u> kama Baba yenu alivyo na huruma. Msihukumu nanyi hamtahukumiwa; msilaumu, nanyi hamtalaumiwa; achilieni nanyi mtaachiliwa."*

Yakobo ameonya kufanya hukumu pasipo huruma. Yakobo 2:13, *"Maana hukumu haina huruma kwake yeye asiyeona huruma. Huruma hujitukuza juu ya hukumu."*

Kama tukifanya hukumu bila kuonyesha huruma, basi hakuna huruma itakayoonyeshwa wakati tutakapo hukumiwa! Kama jinsi Yesu alivyosema katika mustari wa 2: Math. 7:2, *"Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa."* Kwa kipimo kile unachotumia, ndicho utakachopimiwa.

Haimaanishi kwamba hatupaswi kuhukumu, bali tunapohukumu, kumbuka kwamba tutahukumiwa kwa viwango vile vile tunavyotumia! Tuache huruma na upendo vitawale *hukumu zetu.*

Yesu anasema kwamba kuna nyakati ambazo ni "lazima" tufanye hukumu!

Ni "baada" ya kujichunguza sisi wenyewe na kurekebisha makosa yetu.

Kwanza, lazima tutoe "boriti" katika macho yetu wenyewe. Math. 7:5, *"Mnafiki wewe itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe, ndipo utakapoona vema kukitoa kibanzi katika jicho la ndugu yako."*

Baada ya kufanya hivyo, tunakuwa tayari kwa kuona tunakuwa tayari kuchagua (hukumu), na kuwa msaada kwa wale waliochukuliwa kwa makosa yao. Hakika, "sheria ya Kristo" inatutaka tu! Wagal. 6:1-2, *"Ndugu zangu mtu akighafilika katika kosa lo lote ninyi mlio wa Roho mrejezeni mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe. Mchukuliane mizigo hivyo kuitimiza sheria ya Kristo.*

Tena, tunatakiwa kuhukumu kati ya wale walio "*bora*" na wale walio "*nguruwe*" na "*mbwa*".

Chunguza kwa makini maneno ya Yesu katika Math. 7:6, *"Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, wakageuka na kuwararua."* Kuangalia ni nani anayehitaji "hukumu" juu ya sehemu yetu!

Na wale ambao wanapokea, lazima tuwe na uvumilivu katika kujaribu kuwa saidia ili watoke katika makosa yao. Sikiliza kile ambacho Paulo alisema kinahitajia: 2 Tim. 2:24-26, *"Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa <u>mgomvi;</u> bali kuwa <u>mwanana kwa watu wote</u>, awezaye kufundisha, <u>mvumilivu</u>; akiwaonya kwa <u>upole</u> wao washindanao naye, ili kama ikiwezekana, Mungu awape kutubu na kuijua kweli; wapate tena fahamu zao, na kutoka katika mtego wa ibilisi, ambao hao wametegwa naye, hata kuyafanya mapenzi yake."*

Na kwa wale wasiopokea hatutakiwi kuharibu kile ambacho ni kizuri na takatifu kwao! Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kutokupoteza

muda wao kwa kile ambacho si muhimu. Math. 10:12-15, *"Nanyi mkiingia katika nyumba isalimuni. Na nyumba ile ikistahili, amani yenu na iwarudie ninyi. Na mtu asipowakaribisha wala kuyasikiliza maneno yenu, mtokapo katika nyumba ile, au mji ule, kung'uteni mavumbi ya miguuni mwenu. Amini, nawambia itakuwa rahisi kwa nchi ya Sodoma na Gomora kustahili adhabu ya siku ya hukumu, kuliko mji ule."*

Paulo aliwaambia Wayahudi kule Antiokia kwamba walikuwa hawafai kwa ajili ya uzima wa milele. Matendo. 13:42-46, *"Na walipokuwa wakitoka, wakawasihi waambiwe maneno haya sabato ya pili. Sinagogi ilipofumukana, Wayahudi na waongofu watauwa wengi wakashikamana na Paulo na Barnaba, ambao wakisema nao, wakawatia moyo kudumu katika neema ya Mungu. Hata sabato ya pili, watu wengi karibu mji wote, wakakusanyika walisikie neno la Mungu. Bali Wayahudi, walipowaona makutano, wakajaa wivu wakayakanusha maneno yaliyonenwa na Paulo wakibisha na kutukana. Paulo na Barnaba wakanena kwa ushujaa, wakasema ilikuwa lazima neno la Mungu linenwe kwenu kwanza, lakini kwa kuwa mnalisukumia mbali, na kujiona nafsi zenu kuwa hamkustahili uzima wa milele, angalieni twawageukia mataifa."*

Vipi kuhusu hukumu isiyofaa au huduma?

Wengine wanaweza kufikiria kwamba wamehukumiwa isivyostaili kuhudumiwa vibaya na mshiriki wa kanisa na wanataka kulipiza kisasi.

Acha nikuambie kuhusu baadhi ya Wakristo ambao wanahudumiwa vibaya. Wakristo wengi wa kwanza walikuwa watumwa wa wakuu ambao hata hawakuwa Wakristo. Wengine walivuka mipaka na kujaribu au kufikiria uhusiano wa uovu dhidi ya wakuu wao kwa sehemu. Baadhi ya watumwa hawa walikuja kwa Petro wakilia na kutaka afanye kitu kuhusu swala hili. Bila shaka, walishangazwa na jibu lake. Petro alifundisha kwamba walitakiwa kuwa wapole na wavumilivu kwa kila ubaya ambayo wangepata kutoka katika mikono ya wakuu wao. 1 Petr. 2:18-24, *"Enyi watumishi, watiini bwana zenu kwa hofu nyingi, sio wao waliowema na wenye upole tu, bali nao waliowakali. Maana huu ndio wema hasa mtu akivumilia huzuni kwa kumkumbuka Mungu pale ateswapo isivyo haki. Kwa maana ni sifa gani kustahimili, mtendapo dhambi na kupigwa makofi? Lakini kustahimili mtendapo mema na kupata mateso huu ndio wema hasa mbele za Mungu. Kwa sababu ndio mlioitiwa, maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo mfuate nyayo zake. Yeye hakutenda dhambi wala hila haikuonekana kinywani mwake. Yeye alipotukanwa hakurudisha matukano, alipoteswa hakuogofya; bali alijikabithi kwake yeye ahukumuye kwa haki. Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika*

mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki, na kwa kupigwa kwake mliponywa."

Hatakama walikuwa Wakristo hawakuwa na haki. Wangeweza kupigwa, kuburuzwa, kukatwa lakini walitakiwa wavumilie. Petro anasema wasingeweza kuita ukweli kwamba ni Wakristo ili majonzi yao yakome, lakini walipaswa kuvumilia, mateso hata kwa ubaya.

Yesu Kristo alipitia mateso na ni mfano wetu jinsi tunavyo weza kuchukua uamzi tunapofikiria tunateseka bila makosa, vile vile.

Filemoni, hataivyo, alikuwa Mkristo aliyekuwa na watumwa (au hata mmoja, Onesmo). Onesmo hakuwa Mkristo, sanasana kabla ya wakati alipomuacha Filemoni na kutorokea Rumi wakati ambapo alikutana na Paulo ambaye alikuwa kifungoni kwa wakati huo.

Sasa, wengi walikuwa watumwa kwa sababu ya kukamatwa wakati wa vita. Wengine walizaliwa wakiwa watumwa, wazazi wao wakiwa watumwa. Wengine walifanywa watumwa kwa kupenda wengine walikwa wanadaiwa au kwa sababu ya makosa waliokuwa wamefanya. Naamini ni kwa sababu ya barua katika swala la Onesimo, sababu Paulo alisema: Filemoni 1:18-19*, "Na kama amekudhulumu au unamwia kitu, ukiandike hicho juu yangu. Mimi Paulo nimeandika kwa mkono wangu mwenyewe mimi nitalipa. Sikuambii kwamba nakuwia hata nafsi yako."*

Onesimo alikuwa ni mfungwa aliyetoroka. Kwa sababu hii, kwa ajili ya sheria ya Rumi, angeweza kupigwa vibaya na kuwekewa alama ya moto kama mwizi. Onesimo angefanya nini kama mtumwa aliyetoroka? Yaweza kuwa alisikia kuhusu Paulo, aliyefundisha habari za Yesu Kristo kule nyumbani kwao, na kumshawishi Filemoni na wengine kuwa Wakristo, alishikwa na kupelekwa Rumi. Bila shaka, alikwenda kwa Paulo kutafuta ushauri.

Kwa wakati huo Onesimo alikuwa pamoja na Paulo pia alifanyika kuwa Mkristo. Paulo alimtuma Onesimo kurudi kwa Filemoni na barua akiomba msamaha kwa niaba ya Onesimo na ampokee kwa sababu amempata ndugu katika Kristo; kwamba atakuwa zaidi sana na faida kwake yeye na kwa Paulo wakifanya kazi kama Wakristo. Filemoni 1:11, *"Ambaye zamani alikuwa hakufai, bali sasa akufaa sana, wewe na mimi pia;"*

Filemoni angehitaji haki yake kama aliyekuwa na mtumwa. Paulo akamwomba aweke haki hizo pembeni kwa sababu ya Kristo. Kwa sababu wote walikuwa Wakristo walikuwa na nafasi ya kutimiza mengi kwa ajili ya Bwana.

Baathi leo wanafikiria kwamba wakikosewa wanapeleka mashitaka yao kwenye uongozi wa kidunia, badala ya kusuluhisha matatizo yao wenyewe kama Wakristo. Hii ilitokea hata wakati wa Paulo, na akafundisha juu ya swala hili. 1 Wakor. 6:7-8*, "Basi imekuwa upungufu*

kwenu kabisa, kwamba mnashitakiana ninyi kwa ninyi. Maana si afadhali kudhulumiwa? Maana si afadhali kunyang'anywa mali zenu? Basi kinyume cha hayo ninyi wenyewe mwadhulumu watu na kunyang'anya mali zao, naam, hata za ndugu zenu." Sawa na jinsi Petro alivyowaambia Wakristo waliokuwa watumwa.

Paulo alisema niafadhali kupata mateso, kudhulimiwa, kuliko kumshitaki ndugu.

Wakristo wanatakiwa kuwa na tabia hii hata kama si swala la kisheria, bali ni swala la dhamira; hiyo ni, kama haiendi kinyume na sheria ya Kristo. Waru. 14:13, *"Basi tusizidi kuhukumiana, bali afadhali toeni hukumu hii, mtu asitie kitu cha kumkwaza ndugu au cha kumuangusha."* Hukumu, katika swala hili, inahusiana na maswala a,mbayo hayafundishwi katika maandiko – wakati mtu anapoamini kwamba kitu kinakubalika kidini, lakini mwingine akaamini kuwa ni dhambi.

Angalia mfano ambao Paulo anafundisha kuhusu ulaji wa nyama. Waru. 14:14-15, *"Najua tena nimehakikishwa sana katika Bwana Yesu, ya kuwa hakuna kitu kilicho najisi kwa asili yake, lakini kwake yeye akionaye kitu kuwa najisi, kwake yeye kitu kile ni najisi. Na ndugu yako akiingia huzuni kwa sababu ya chakula, umeacha kwenda katika upendo. Kwa chakula chako usimharibu mtu yule ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake."*

Nina shawishiwa kwamba anazungumzia ulaji wa nyama zilizotolewa kwa ajili ya sanamu, kwa sababu alishughulikia somo kama hili kule Korintho kama alivyofanya katika Rumi. 1 Wakor. 8:4-12, *"Basi kwa habari ya kuvila vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, twajua ya kuwa sanamu si kitu katika ulimwengu, na ya kuwa hakuna Mungu ila mmoja tu. Kwa maana ijapokuwa wapo waitwao miungu, ama mbinguni ama duniani, kama vile walivyoko miungu mingi na mabwana wengi; lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake, yuko na Bwana mmoja Yesu Kristo ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo na sisi kwa yeye huyo. Bali ujuzi huu haumo ndani ya watu wote; ila wengine kwa kuizoelea ile sanamu hata sasa hula kana kwamba ni kitu kilichotolewa kwa sanamu, na dhamiri zao kwa kuwa dhaifu, hunajisika. Lakini chakula hakituurishi mbele za Mungu, maana tusipokula hatupunguziwi kitu, wala tukila hatuongezewi kitu. Lakini angalieni huu uwezo wenu usije ukawakwaza wale walio dhaifu. Kwa maana mtu akikuona wewe uliye na ujuzi, umeketi chakulani mbele ya hekalu la sanamu, je! Dhamira yake mtu huyo, kwa kuwa yu dhaifu, haitadhibitika hata yeye naye ale vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu? Na Yule aliye dhaifu aangamizwa kwa ujuzi wako, naye ni ndugu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake. Hivyo mkiwatenda dhambi*

ndugu zenu na kuitia jeraha dhamiri iliyo dhaifu mnamtenda dhambi Kristo."

Bwana wetu alimwambia Petro kwamba ilikuwa sahihi kula nyama ambayo mwanzoni ili katazwa chini ya sheria ya Musa. Matend. 10:9-17, *"Hata siku ya pili walipokuwa wakisafiri na kuukaribia mji, Petro alipanda juu darini, kwenda kuomba yapata saa sita ya mchana; akaumwa na njaa sana akataka kula; lakini walipokuwa wakiandaa, roho yake ikazimia, akaona mbingu zimefunuka, na chombo kikishuka kama nguo kubwa, inatelemshwa kwa pembe zake nne hata chini; ambayo ndani yake walikuwamo aina zote za wanyama wenye miguu minne, na hao watambaao, na ndege wa angani. Kisha sauti ikamjia, kusema, ondoka, Petro uchinje ule. Lakini Petro akasema, Hasha, Bwana, kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au najisi. Sauti ikamjia mara ya pili, ikimwambia, Vilivyotakaswa na Mungu, usiviite wewe najisi. Jambo hili likatendeka mara ya tatu; kisha kile chombo kikapokewa tena mbinguni. Hata Petro alipokuwa akiona shaka ndani ya nafsi yake, maana yake ni nini maono hayo aliyoyaona, wale watu waliotumwa na Kornelio, wakiisha kuiulizia nyumba ya Simoni, wakasimama mbele ya mlango."*

Sasa, kwa vile Yesu alisema ni vema kula nyama, siamini kwa ulaji wa nyama ilikuwa ni tatizo. Kama nilivyosema, hata hivyo, kulikuwa na baadhi katika wakati wa Paulo waliofikiri kuwa ni dhambi kula nyama ambayo labda ilitolewa sadaka kwa sanamu. Alisema hili lili kuwa ni tatizo la dhamira ya ndugu ye yote kwamba asile, na mwingine kuwa huru kwamba aweze kula.

Paulo alijisemea yeye mwenyewe, 1 Wakor. 8:13, *"Kwa hiyo chakula kikimkwaza ndugu yangu, hakika sitakula nyama hata milele, nisije nikamkwaza ndugu yangu."* Kumbuka, Paulo aliliweka wazi kwa Wakorintho kwamba amekuwa akizungumzia nyama ambazo labda zilikuwa zimetolewa sadaka kwa sanamu.

Kwa sababu tu unaamini kwamba unaweza ukawa na haki ya kufanya kitu, haimaanishi kwamba unapaswa kuifanya, kama dhamira ya ndugu yako ikiathiriwa. Paulo alisema katika 1 Wakor. 6:12, *"Vitu vyote ni halali kwangu, lakini si vyote vifaavyo; vitu vyote ni halali kwangu lakini, lakini mimi sitatiwa chini ya uwezo wa kitu cho chote."* Hiyo ni, vitu vyote ambavyo havija kuwa chini ya sheria ya Kristo, lakini tunapaswa kuwapenda ndugu zetu viakutosha ili tusiwavunje moyo.

Mwisho

Aina ya hukumu ambayo Yesu amekataa na akatilia maanani, ni hukumu ya kinafiki ambayo si ya ukweli na kuiita hukumu ya Mungu juu ya mtu binafsi. Hii ndiyo aina ya hukumu ambayo pia ili kataliwa na Yakobo alipoandika: Yakob. 4:11-12, *"Ndugu msisingiziane, amsingiziaye ndugu yakeau kumhukumu ndugu yake, husingizia sheria na kuihukumu sheria. Lakini ukiihukumu sheria, huwi mtenda sheria, bali umekuwa hakimu. Mtoa sheria na mwenye kuhukumu ni mmoja tu, ndiye awezaye kuokoa na kuangamiza. U nani wewe umuhukumuye mtu mwingine?*

Hii inamaanisha kuongea mabaya juu ya watu wengine na kufanya hukumu bila kujua ukweli wote; labda kueneza habari ambayo labda siyo ya kweli kati ya ndugu. Mungu na atusaidie kuondokana na aina hiyo ya hukumu; kuwa tayari kuondoa "*boriti*" katika macho yetu wenyewe; ili tuweze kuwa tayari kuwasaidia wengine katika shida zao.

Lakini kusema hatupaswi kuhukumu kabisa, ni kudharau kile ambacho Yesu alifundisha, siyo tu katika kifungu hiki bali hata katika vifungu vingine pia!

Hata hivyo, tunatakiwa tuwe makini katika kuhukumu maswala ya dhamira katika mambo ambayo hayaja zungumzwa na sheria ya Kristo.

Kuongelea hukumu, je umejiandaa binafsi kwa siku ambayo utahukumiwa na Bwana? Yoh. 12:48, *"Yeye anikataaye mimi asiyekubali maneno yangu, anaye amuhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho."* 2 Wakor. 5:10, *"Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya."*

Kumbuka sisi ni wahudumu (watumwa) wa Bwana. Tukiwa tumetoa huduma yetu na kutoka kwake, adhabu itakuwa mbaya kwetu kuliko ya mtumwa aliyetoroka. 2 Petr.2:20-21, *"Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua kisha kuiacha ile amri takatifu waliopewa."*

Hebu tuchukue kazi ya Bwana kwa makini.